

SEKONDARI MSINGI

MUHUWA 2

MTIHANI WA KWANZA

# MWONGOZO WA USAHIIHISAJI.

Chagua jina au majina mwafaka kujaza mianya kwa kuchagua kwenyewe kijisanduku hiki.  
(alama 5)

Kwa kweli dawa ya moto ni **moto**. Jambazi **lile** lilikuwa **limemkamata** mwenye duka ili **limpore** mali yake yote. **kwani** lilipoingia, lilimwonyesha bastola na kumwamrisha alale chini. Punde si punde **umati** wa watu ulivamia jambazi lile na kuliua papo hapo.

**Limpore**



**moto**

Download this and other FREE materials from <https://teacher.co.ke/notes>



file

Limemkamata

Download this and other FREE materials from <https://teacher.co.ke/notes>



umati

Download this and other FREE materials from <https://teacher.co.ke/notes>



kwani

Download this and other FREE materials from <https://teacher.co.ke/notes>



## **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Inasikitisha kuona yakwamba visa vya uhalifu vinazidi kuongezeka katika taifa letu **kila uchao**. Wahuni wanashiriki katika visa hivi bila kujali athari na maafa wanayosababisha.

Hebu vuta taswira uone jinsi uhalifu unavyosababisha hasara chungu. Watu hupoteza maisha yao. Mathalani uhalifu wa magaidi ambao hulipua majumba makubwa pasi kujali wala kubali huwafanya wengi kulala usingizi usiojua asubuhi. Watu wenye taaluma hujificha tu kama nzige waliopuzwa dawa. Watu hawa huendesha uchumi wa nchi. Wao ni kama kitegauchumi.

Tazama mali ambayo huharibiwa majumba yale yanapoporomoka au kuteketea. Hayahesabiki wamiliki wa mali hiyo hubaki mdomo achama wayaonapo yamebaki majivu. Utakubaliana nami kuwa jambo hili linaatua moyo. Uhalifu sio tu wa magaidi, kuna wizi, ubakaji, udanganyifu nikitaja machache tu.

Basi tufanyeje kama wanainch kuukomesha halifu huu ? Tuungane mikono maana jifya moja haliinjiki chungu. Tueleze wakembe wetu maadili bora tangu wakiwa wana kwa kuwa kamarare mkunje akiwa mbichi. Nao watazifuata nyendo nyoofu hata wakibaleghe. Wanaokaidi amri, waadhibiwe mapema tusije tukajenga ukuta badala ya kuurekebisha ufa.

### **Maswali.**

Kulingana na taarifa, kwa nini kuna sikitiko ? **(Alama 2)**

### **Visa vya uhalifu vinazidi kuongezeka**

Kauli 'kila uchao' kama ilivyotumika katika kifungu ina maana gani ? **(Alama 2)**

### **Siku zinapoenda ama kila siku mpya inapokucha**

Jifya moja haliinjiki chungu ni fani gani ya lugha ? **(Alama 2)**

### **methali**

Zifuatazo ni athari za uhalifu ispokuwa **uchumi kuimarika (Alama 2)**

**(mauko, mali kuharibika, uyatima, uchumi kuimarika)**

### **Uchumi kuimarika**

Kwa nini wahalifu wanastahili kuchukuliwa hatua baada ya kupatikana ? **(Alama 2)**

### **Uhalifu unasabbisha vifo, uharibifu wa mali**

Mwandishi ametaja njia ngapi za uhalifu ? **(Alama 2)**

### **nne**

Methali 'jifya moja haliinjiki chungu' imetumika katika makala. Ni methali ipi ni kisawe chake ?

**(Alama 2).**

### **Kidole kimoja hakiui chawa**

**Kamilisha maamkuzi yafuatayo.**

**(Alama 5)**

**Maamkuzi**

**maagano**

a.) Alamsiki

**binuru**

b.) Sabalkheri

**sabalkeri**

c.) Lala unono

**nawe pia**

d.) Hujambo

**sijambo**

**Andika sentensi hii kwa wingi :**

**(Alama 5)**

Punda amebeba mzigo mzito.

**Punda wamebeba mizigo**

**Kanusha sentensi :**

**(Alama 5)**

Chakula cha mtoto kimeiva.

**Chakula cha mtoto hakijaiva**

**Tambua vipengele vitano katika usikilazaji wa mazungumzo**

**(Alama 5)**



**Kuskiliza kwa makini.**



**Kumtazama mzungumzaji kwa makini ili kupata ishara za uso.**



**Kutikisa kichwa ili kuonyesha kukubali.**



**Kutumia maneno ya kumhimiza mzungumzaji kuendelea kuzungumza.**



**Kumtazama mzungumzaji ana kwa ana.**



**Kutumia lugha ya adabu katika mazungumzo.**

Orodhesha sehemu **nne** ambapo herufi kubwa hutumika.

**(Alama 4)**



**Mwanzoni mwa sentensi.**



**Mwanzoni mwa nomino za pekee.**



**Kuandika kichwa au mada.**



**Kuandika vifupisho**